

## Fahamu hatari za kutumia mwakilishi asiye na kibali

Kila mwaka, mamia ya maelfu ya watu wanachagua kuifanya nchi ya Canada kuwa makazi yao. Wengi wa wageni hawa huamua kuajiri mwakilishi wa kuwasaidia kushughulikia mchakato wa uhamiaji au uraia.

Ukijiri mwakilishi, lazima awe na kibali cha [College of Immigration and Citizenship Consultants](#). Immigration, Refugees and Citizenship Canada (IRCC) itashughulika tu na wawakilishi wenyewe kibali cha kutoa ushauri au uwakilishi wa masuala ya uhamiaji kwa malipo. **IRCC haitakubali maombi yanayowasilishwa na wawakilishi wasio na vibali.**

### Kuajiri mwakilishi asiye na kibali inaweza kuwa na madhara makubwa

Jihadharishe na watu wanaojiita wawakilishi wa masuala ya uhamiaji wasio na kibali cha Chuo cha Wataalamu wa maswala ya Uhamiaji na Uraia. Wawakilishi wasio na vibali wanaweza kukosa mafunzo au elimu sawa na wawakilishi wenyewe vibali au wawakilishi wengine wanaolipwa (wanasheria na wathibitishaji wa hati za kisheria).

Wawakilishi wasio na vibali hawana maadili sawa na wanachama wa Chuo. Ndiyo maana kutumia mwakilishi asiye na kibali inaweza kuleta madhara makubwa, kama vile:

- kupoteza fedha zako:
  - kulipia huduma gushi
  - kulipia huduma za ulaghai
- maombi yako kukataliwa:
  - mwakilishi asiye na kibali anakuambia utume maombi kwenye programu ambayo huna ustahiki nayo, kwa hiyo maombi yako yanakataliwa
- kupigwa marufuku kuingia nchini Canada:
  - mwakilishi asiye na kibali anayekupotosha kuficha taarifa fulani kwenye maombi yako, na mwishowe kupigwa marufuku kuingia nchini Canada kwa miaka mitano.

Kutumia mwakilishi asiye na kibali inaweza pia kusababisha

- wizi wa utambulisho
- fedha kuibwa kwenye akaunti yako ya benki au kadi ya mkopo au kadi ya kiotomotela
- vitisho vya unyanyasaji
- dhuluma

Kwa taarifa zaidi kuhusu kubaini, kuepuka na kuripoti vitendo vya ulaghai, tembelea tovuti ifuatayo: [Canada.ca/immigration-fraud](https://Canada.ca/immigration-fraud).

Ili kuhakikisha mwakilishi wako wa masuala ya uhamiaji au uraia ameidhinishwa, tembelea tovuti ifuatayo: [Canada.ca/immigration-representative](https://Canada.ca/immigration-representative).